TANGAZO LA SERIKALI Na. 381 la tarehe 15/5/2020

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)

(SURA. 287)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya kifungu cha 153(1))*

SHERIA NDOGO YA UANZISHAJI WA MFUKO WA AFYA YA JAMII (TIBA KWA KADI) YA HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME YA MWAKA 2020

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina la sheria

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Uanzishaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii (Tiba kwa Kadi) ya Halmashauri ya Wilaya ya Same ya Mwaka 2020.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Same.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi, isipokuwa kama itaelezwa vinginevyo-

“Bodi” maana yake ni chombo kinachosimamia huduma za afya katika Halmashauri;

“Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Same;

“huduma za afya” maana yake ni huduma zote za afya zinazotolewa na hospitali, vituo vya afya, zahanati na kliniki maalum zinazomilikiwa na Serikali, Mashirika ya dini, mashirika yasiyo ya Serikali au watu binafsi;

"kadi" maana yake ni kadi itakayotolewa kwa mwanachama wa Mfuko wa Afya ya Jamii (Tiba kwa Kadi);

"mchango" maana yake ni mchango wa fedha wa hiari unaotolewa na mwanachama wa Mfuko wa Afya ya Jamii (Tiba kwa Kadi);

"Mfuko" maana yake ni Mfuko wa Afya ya Jamii (Tiba kwa Kadi);

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya y a Same au afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi"

"mwanachama" maana yake ni mtu au kaya yeyote inayochangia Mfuko wa Afya ya Jamii (Tiba kwa Kadi).

## SEHEMU YA PILI

## MAJUKUMU YA MFUKO WA AFYA YA JAMII (TIBA KWA KADI) NA KAMATI YA AFYA YA KATA

Mfuko wa Afya ya Jamii (Tiba kwa Kadi)

4. Kutakuwa na Mfuko wa Afya ya Jamii (Tiba kwa Kadi) ambao utakuwa ni wa hiari wenye lengo la kugharamia kutoa huduma za afya kwa wanachama,

Madhumuni

5. Mfuko utakuwa na madhumuni yafuatayo:
   (a) kuimarisha huduma za afya katika jamii kwa kuhakikisha jamii inachangia upatikanaji wa huduma za afya na kuwa na nguvu ya kufanya maamuzi kuhusu masuala yanayohusu afya;
   (b) kuweka mipango endelevu ya utoaji wa huduma bora za afya; na
   (c) kutafuta rasilimali fedha kwa ajili ya kuimarisha utoaji wa huduma bora za afya.

Majukumu ya Bodi ya

6.- Bodi ya Huduma ya Afya ya Halmashauri

Huduma za Afya Sura 409

iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mfuko wa Afya ya Jamii itakuwa na wajibu wa kusimamia utoaji wa huduma za afya katika Halmashauri.

Akaunti ya Mfuko

7.- (1) Kutakuwapo na Akaunti ya Mfuko itakayotumiwa na Halmashauri ambamo fedha zote zitakazokusanywa kwa ajili ya Mfuko zitahifadhiwa.

(2) Wawekaji wa saini wa Akaunti ya Mfuko watakuwa ni Mwenyekiti wa Bodi au mjumbe wa Bodi mmoja atakayeteuliwa na Bodi kwa upande mmoja na Katibu wa Bodi au mweka hazina wa Halmashauri kwa upande mwingine.

Vyanzo vya mapato ya Mfuko

8. Vyanzo vya mapato ya Mfuko vitakuwa ni-

(a) fedha zote zinazotokana na michango ya wanachama;
(b) ruzuku kutoka Halmashauri na Serikali Kuu;
(c) wahisani mbalimbali toka ndani na nje ya Halmashauri;
(d) michango ya watu binafsi wanaoishi ndani na nje ya Halmashauri;
(e) ushuru unaotozwa na Halmashauri kutoka vyanzo mbalimbali na kutengwa kwa ajili ya Mfuko;
(f) Mchango kutoka Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya; na
(g) fedha zozote halali ambazo Mfuko unaweza kupata toka mahali pengine popote.

Matumizi ya fedha za Mfuko

9. (1) Fedha zitakazokusanywa na Mfuko zitatumika katika-

(a) masuala yanayohusu afya yaliyotajwa katika mpango kabambe wa afya wa

Halmashauri; na

(b) suala au shughuli yoyote muhimu ya afya itakayoidhinishwa na Bodi.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1), asilimia themanini ya mapato ya tele kwa tele itabaki kwenye akaunti ya Mfuko na asilimia ishirini itarudi kwenye vituo vya afya kwa ajili ya matumizi ya vituo hivyo.

Usimamizi wa Mfuko

10. Usimamizi na uendeshaji wa Mfuko utakuwa kama ifuatavyo:

(a) katika ngazi ya Halmashauri, utakuwa chini ya Bodi;

(b) katika ngazi ya Kata, utakuwa chini ya Kamati ya Maendeleo ya Kata kupitia kamati za afya za vituo husika;

(c) katika ngazi ya Mtaa, utakuwa chini ya Kamati ya Mtaa kupitia Kamati ya Huduma za Jamii.

Taarifa ya fedha na ukaguzi

11.- (1) Bodi itakuwa na wajibu wa kuwasilisha taarifa za fedha za Mfuko kwa Halmashauri kila robo mwaka na taarifa ya mwaka itakayowasilishwa mwezi mmoja baada ya kumalizika kwa mwaka wa fedha.

(2) Hesabu za fedha za Mfuko zitakaguliwa kila mwaka kwa kuzingatia taratibu za ukaguzi wa fedha za umma.

Mipango

12.- Mipango ya makadirio ya mapato na matumizi ya Mfuko itaandaliwa, kuchambuliwa na kuidhinishwa na Bodi kabla ya kuwasilishwa katika Halmashauri kwa kuzingatia ratiba ya vikao vya bajeti vya Halmashauri.

Mratibu wa Mfuko

13.- (1) Kutakuwa na Mratibu wa Mfuko wa Afya ya Jamii (Tiba kwa Kadi) wa Halmashauri atakayeteuliwa na Mkurugenzi baada ya kushauriwa na timu ya uendeshaji ya

Halmashauri.

(2) Mratibu wa Mfuko atakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) kufuatilia, kusimamia na kuratibu uendeshaji wa Mfuko kwenye vituo vya kutolea huduma za afya;

(b) kuwa kiungo kati ya Halmashauri, jamii na wadau mbalimbali;

(c) kuandaa taarifa za Mfuko za robo na za mwaka pamoja na majukumu mengine atakayopangiwa na Mkurugenzi; na

(d) kuhudhuria vikao vyote vya Bodi na kutoa taarifa za utekelezaji wa shughuli za Mfuko.

Majukumu ya Kamati ya Afya ya Kata Sura 409

14. Kamati ya Afya ya Kata iliyoundwa kwa mujibu wa Sheria ya Mfuko wa Afya ya Jamii itakuwa na majukumu yafuatayo

(a) kuhamasisha na kuandaa jamii kujiunga na Mfuko;

(b) kuandaa orodha ya wanachama wa Mfuko na kufuatilia idadi ya wanachama;

(c) kusimamia ukusanyaji wa michango ya Mfuko;

(d) kuratibu viwango vya uchangiaji wa Mfuko;

(e) kupitia utendaji wa Mfuko na kutoa mapendekezo ya kuimarisha utendaji kwa Halmashauri kupitia Bodi;

(f) kubuni na kuratibu mipango ya afya ya jamii; na

(g) kuratibu mikutano ya wanachama wa Mfuko katika eneo la Kata.

Wajumbe wa Kamati ya Afya ya Kata

15. (1) Kamati ya Afya ya Kata itakuwa na wajumbe wafuatao-

(a) diwani anayewakilisha kata husika;

(b) afisa mtendaji wa kata;

(c) mwalimu mkuu mmoja kutoka kwenye Shule ya Msingi ambayo ipo kwenye Kata husika;

(d) wajumbe wawili watakaowakilisha jamii husika ambapo mmoja wao ni lazima awe mwanamke;

(e) Tabibu mfawidhi au tabibu mfawidhi msaidizi; wa kituo cha afya au zahanati, ambaye atakuwa katibu wa Kamati;

(f) mjumbe mmoja atakayeteuliwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata kutokana na watu waliopendekezwa na Kamati za Kata husika; na

(g) mjumbe mmoja atakayeteuliwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata kutoka kwenye vyama vya kijamii kutoka kwenye Kata husika.

(2) Mwenyekiti wa Kamati ya Afya ya Kata atachaguliwa kutoka miongoni mwa wajumbe lakini asiwe diwani,Mtendaji wa Kata au mtendaji wa Mtaa.

## SEHEMU YA TATU
## UANACHAMA WA MFUKO

Uanachama wa Mfuko

15.- (1) Mtu au kaya yoyote itakayotaka kuwa mwanachama wa Mfuko wa Afya ya Jamii (Tiba kwa Kadi) itatakiwa kulipa kila mwaka mchango wa uanachama wa shilingi elfu thelathini.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1), Halmashauri itakuwa na wajibu wa kulipa ada ya uanachama wa Mfuko wa kaya masikini baada ya kaya husika kupendekezwa na Kamati ya Afya ya Kata na kuidhinishwa na Bodi.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) na (2), kila mtu au kaya iliyolipia mchango wa uanachama itapewa kadi za

uanachama.

(4) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), Halmashauri inaweza kubadilisha kiwango cha mchango wa uanachama wa Mfuko, baada ya kutoa taarifa kwa mwanachama.

Ukomo wa uanachama

16. Mtu au kaya itakoma kuwa mwanachama wa Mfuko endapo itashindwa kulipa mchango wa uanachama ndani ya muda wa siku sitini tangu kumalizika kwa kipindi cha mwaka mmoja kilicholipiwa mchango.

Haki za mwanachama

17. Kila mwanachama atakuwa na haki ya-

(a) kupata huduma ya afya aliyolipia kabla ya kuugua ndani ya eneo la Halmashauri au eneo lingine lolote kadri itakavyokubaliwa;

(b) kutoa mapendekezo kuhusu huduma za afya kupitia Kamati ya Afya ya Kata ambayo yatafanyiwa kazi na Bodi; na

(c) kushirikishwa kikamilifu katika uandaaji na utekelezaji wa mpango wa upatikanaji wa huduma za afya katika eneo la Halmashauri.

SEHEMU YA NNE
MASUALA MENGINEYO

Malipo ya papo kwa papo

18. (1) Mtu yeyote ambaye hatakuwa mwanachama wa Mfuko au mwanachama wa mfuko mwingine atalipa malipo ya papo kwa papo kila atakapoenda kupata matibabu katika kituo cha kutolea huduma za afya kwa viwango vifuatavyo:

(a) shilingi elfu mbili kwa huduma za afya zinazotolea katika zahanati katika eneo

lolote la Halmashauri;

(b) shilingi elfu tatu kwa huduma za afya zinazotolewa na kituo cha afya kilichopo ndani ya Halmashauri;

(c) kiasi kitakachopangwa kwa mujibu wa Sera ya Afya na miongozo itakayotolewa kwa huduma za afya zinazotolewa na hospitali.

Utaratibu wa msamaha

19. Msamaha kwa wasioweza kulipia gharama za matibabu utatolewa na kulipiwa na Halmashauri baada ya-

(a) Kamati ya Mtaa au Halmashauri ya Kijiji kuwatambua, kuwajadili na kuwasilisha mapendekezo ya orodha ya majina ya watu wanaostahili kupewa msamaha kwenye Kamati ya Maendeleo ya Kata;

(b) Kamati ya Maendeleo ya Kata kuwajadili wale wasioweza kulipia gharama na kuthibitisha orodha yao na kuiwasilisha kwenye Bodi; na

(c) Bodi kujadili mapendekezo husika na kuyawasilisha pamoja na gharama zake kwa Halmashauri kwa ajili ya kulipiwa.

Kamati za Afya za Zahanati

20. Kamati ya Afya ya Zahanati na Kamati zote ziliundwa chini ya Hati Rasmi ya Uanzishaji wa Bodi, zitafanya kazi na Mfuko huu kwa kuzingatia Sheria Ndogo hii.

Mhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Same umebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa Azimio lililopitishwa na mkutano wa baraza la Madiwani ulioitishwa tarehe 15/3/2018.

ANNA CLAIRE SHIJA
*Mkurugenzi,*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Same*

CHRISTOPHER M. IRIRA,
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Same*

NAKUBALI,

L.S

*Dodoma,*
16 Aprili, 2020

SELEMANI S. JAFO (MB.),
*WN OR-TAMISEMI*
*Dodoma*